
# 坦桑尼亚联合共和国

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# 教育科技部

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



坦桑尼亚联合共和国
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
教育科技部
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

许可证
Cheti cha Ithibati

编号Na. 1097

大纲名称：小学汉语教学技能文凭培训大纲
Jina la Chapisho: Muhutasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kichina Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

出版机构：坦桑尼亚教育学院
Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

作者：教育科技部
Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-847-7

本教学大纲已于2023 年6月29号获得教育科技部批准，作为坦桑尼亚小学汉语教学技能文凭培训大纲。

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kichina Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa 博士
Kamishna wa Elimu 教育专员

# 小学汉语教学技能文凭培训大纲

# MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KICHINA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

**2023 年**

© 2023 坦桑尼亚教育研究院
2023 年第一版

书号: 978-9987-09-847-7

坦桑尼亚教育研究院
Mikocheni 地区
Ali Hassan Mwinyi 路 132 号
邮政信箱：35094
14112 达累斯萨拉姆

电话: +255 735 041 168/+255 735 041 170
邮箱: director.general@tie.go.tz
网址: www.tie.go.tz

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023
Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-847-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan
S.L.P 35094
14112 Dar es salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

引用本大纲请注明来源为：教育科技部。(2023)。小学汉语教学技能文凭培训大纲。坦桑尼亚教育研究院。
Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia. (2023). *Muhtasari wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kichina Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

版权所有。未经坦桑尼亚教育研究院书面许可，不得以任何形式复制、转载、出版、翻译或赠送本大纲。
Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania

# 目录Yaliyomo

表目录Orodha ya majedwali ........ iv
缩略词Vifupisho ........ v
致谢Shukrani ........ vi
1.0 简介Utangulizi ........ 1
2.0 教育的总目标Malengo Makuu ya Elimu nchini Tanzania ........ 1
3.0 教师教育目标 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2
4.0 文凭课程教学的综合能力Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu ........ 3
5.0 中文课程的主要能力和具体能力 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Lugha ya Kichina ........ 4
6.0 讲师、师范生和家长/监护人在小学汉语教学过程中的角色Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi/Mlezi katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
6.1 讲师Mkufunzi ........ 6
6.2 师范生Mwalimu Tarajali ........ 7
6.3 家长/监护人Mzazi/Mlezi ........ 8
7.0 教学方法Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8
8.0 教学工具/设备Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 9
9.0 学习进度评估Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ........ 9
10.0 课时数量Idadi ya Vipindi ........ 11
11.0 教学内容Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 11
第一年Mwaka wa Kwanza ........ 12
第二年Mwaka wa Pili ........ 28
参考文献Bibliografia ........ 30

## 表目录Orodha ya majedwali

表 1：Jedwali 1: 受训教师的主要能力和具体能力Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Mwalimu Tarajali ..........................5

表 2：Jedwali 2: 持续评估标志计划 Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu ........................................................10

表 3：Jedwali 3： 第一年教学内容 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Mwaka wa Kwanza .............................12

表 4：Jedwali 4: 第二年教学内容 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Mwaka wa Pili.......................................28

## 缩略词Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | 坦桑尼亚手语Lugha ya Alama Tanzania |
| TEHAMA | 信息与通信技术 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | 坦桑尼亚教育研究院Taasisi ya Elimu Tanzania |

# 致谢Shukurani

《小学汉语教学技能文凭培训大纲》的编写，涉及到来自公共和私营机构的各种专业人员。坦桑尼亚教育研究院（TET）衷心感谢所有参与其中的专业人员，包括坦桑尼亚教育研究院的课程开发人员、讲师、培训师、学校质量控制人员、教师以及来自非政府组织的专家。

此外，TET特别感谢由教育科技部长任命的全国专家委员会，负责监督学前、基础、中等和教师教育课程改革工作。该委员会以专业精神工作，确保此大纲的内容符合2023年课程改革的主要目标，即培养具备就业技能、知识和能力的毕业生，使其能够自谋职业、就业并应对日常生活。因此，坦桑尼亚教育学院还特别感谢教育科技部为本大纲的编制和分发提供的支持。

Maandalizi ya muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina stashahada ya ualimu wa elimu ya msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, pamoja na wakuza mitaala wa TET.

Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati kamati ya kitaifa ya wataalamu ya kusimamia kazi ya maboresho ya mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la maboresho ya mitaala ya mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu

Aneth A. Komba 博士
院长
**坦桑尼亚教育研究院**

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 简介Utangulizi

中文教学方法是小学教育文凭课程中将要教授中国语文的教师的必修课。该课程的目标是赋予将要在小学三年级至六年级教授中国语文的师范生各种教学和学习策略。

本教学大纲旨在指导讲师为即将在坦桑尼亚大陆小学三至六年级教授中文的师范生们做好准备。该教学大纲已翻译了2023年小学教育文凭的课程。此外，该教学大纲将使讲师能够规划教学和学习活动，培养师范生在教学和学习环境中的探究力、创造力、合作、沟通和解决问题的能力。Somo la mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina stashahada ya ualimu elimu ya msingi ni la lazima kwa mwalimu atakayefundisha lugha ya Kichina. Lengo la somo hili ni kumwezesha mwalimu tarajali atakayefundisha lugha ya kichina elimu ya msingi darasa la III–VI kumudu mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mkufunzi kumwandaa mwalimu tarajali kufundisha lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III-VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri mtaala wa mafunzo ya stashahada ya ualimu elimu ya msingi wa Mwaka 2023. Pia, muhtasari utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji zitakazomjengea mwalimu tarajali stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 教育的总目标Malengo Makuu ya Elimu nchini Tanzania

坦桑尼亚教育的总目标：Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) 提升和改善个人品格，培养自尊和自信心；
Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini；

(b) 尊重坦桑尼亚的文化、传统和习俗，以及不同的文化观点、人道主义、人权、态度和包容的行为；
Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi；

(c) 学习知识并运用科学技术进行创新，培养批判性思维、创造力、合作沟通和积极的人生态度，在个人发展以及国家和整个世界的可持续发展中发挥作用；
Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla；

(d) 理解并保护国家的核心价值观，包括人性、爱国主义、正直、团结、真诚、诚实、问责和国家语言；
Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa；

(e) 培养生活技能和就业技能，提高日常生活的效率；
Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku；

(f) 倡导以爱和尊重为基础的职业道德，以提高生产和服务提供的生产力和效率；
Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma；

(g) 认识和解决跨领域问题，包括人们（社会）的健康和福祉、性别平等，以及环境的可持续发展和保护；
Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira；

(h) 促进国家和国际合作、和平与正义，遵守国家宪法和国际协议。
Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 教师教育目标 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 教师教育的主要目标 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

教师教育的主要目标是培养一名专业且胜任的教师，能够适应与科学、技术和社会变革相符的教学和学习，以便为塔桑尼亚公民的培养做好准备。这位公民应当具备充足的知识、技能和积极的态度，尊重人权、平等和终身学习。

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

## 3.2 教师教育的具体目标 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

教师教育的目标包括使教师能够

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) 培养对教师教育、教学职业道德、人生价值观和教学基础的理论理解;
Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) 掌握教学方法的技能；Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) 掌握基于能力构建理念的评估和测量方法;
Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) 以学生需求为导向，在教学中促进创新和发现;
Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) 在教学中应用信息通信技术和辅助技术;
Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) 促进及早发现有特殊学习需要的学生并提供适当的干预措施;
Kukuza utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) 加强语言在教学中的应用;
Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) 培养以提升课堂教学、学习和评估为目标的技能（基于课堂研究）。
Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based research*).

## 4.0 文凭课程教学的综合能力Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

教师教育的专科课程的主要能力包括以下几个方面:

Umahiri wa jumla wa Stashahada ya Ualimu ni:

(a) 在教学中运用教学理论和原则；
Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) 能够掌握教学方法；Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) 能够衡量和评估基于能力建设的方法；
Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;

(d) 能够根据学生的需要，在教学中运用创造性的方法创新教学；
Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;

(e) 在教学中使用信息技术和辅助技术；
Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) 确定有学习需求的学生并提供适当的干预；
Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) 在教学中流利地使用相关语言；
Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) 在工作中运用领导技能（教学领导)；
Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*);

(i) 掌握旨在改进教学、学习和测试（基于课堂）的技能。
Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based).*

## 5.0 主要能力和具体能力 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Lugha ya Kichina

本节表 1 中规定的受训教师期望培养的主要能力和具体能力。

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali umebainishwa katika Jedwali Na.1.

表 1：**Jedwali 1:** 受训教师的主要能力和具体能力*Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Mwalimu Tarajali*

| 主要能力<br>**Umahiri Mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri Mahsusi** |
|---|---|
| 1.0 掌握小学汉语教学方法<br>Kumudu Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina katika Elimu ya Msingi | 1.1 分析小学汉语教学方法<br>Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina kwa Elimu ya Msingi |
| | 1.2 掌握基于年级层次的听力教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusikiliza kulingana na ngazi ya darasa husika |
| | 1.3 掌握基于年级层次的口语教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kuzungumza kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika |
| | 1.4 掌握基于年级层次的发音教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha matamshi kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika |
| | 1.5 掌握基于年级层次的词汇教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha msamiati kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika |
| | 1.6 掌握基于年级层次的阅读教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za Kusoma kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika |

| 主要能力<br>**Umahiri Mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri Mahsusi** |
|---|---|
| | 1.7 掌握基于年级层次的写作教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za uandishi kulingana na ngazi ya darasa husika |
| | 1.8 能够在教学中使用技术和其他工具<br>Kumudu matumizi ya teknolojia na vyombo vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji |
| | 1.9 掌握基于年级层次的语法教学方法<br>Kumudu Mbinu za kufundisha Sarufi kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika. |
| | 1.10 掌握协调课外活动的各种方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu mbalimbali katika kuratibu shughuli za nje ya darasa |

## 6.0 讲师、师范生和家长/监护人在小学汉语教学过程中的角色Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

教学和学习依赖于讲师、师范生和家长/监护人之间的紧密合作。他们的职责如下:
Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali, mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 讲师Mkufunzi

讲师应当：Mkufunzi anatarajiwa:

(a) 通过使用各种赋权方法来促进基于21世纪技能培养的教学和学习，使师范生成为学习的中心。推荐的方法是那些有助于发展思维能力、反思能力和从各种来源获取知识以解决教学和学习挑战的方法。Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya

mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) 准备有助于教学和学习的环境，包括筛选工具；
Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) 为每位师范生提供公正和平等的培训；
Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) 确定师范生的特殊需求并提供适当的支持。
Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki。

## 6.2 师范生Mwalimu Tarajali

师范生应当：Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) 全力参与课堂内外的培训活动，以确保在各个领域获得足够的能力，包括学习和教学管理、教学方法和评估方法，以便能够评估学习和教学的成果并加以改进；Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji;

(b) 通过参与附近学校和学院的持续培训，将个人品质、课程准备、教学方法的使用、教学和学习资源的准备和使用，以及学生评估等课堂理论转化为实践；Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishiana kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) 在经验丰富的教师监督下工作一年，以提高教学领域的能力和专业水平；Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) 与同事和导师合作进行学习；Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) 遵守学院的规章制度。Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

## 6.3 家长/监护人Mzazi/Mlezi

家长/监护人应当：Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) 管理和监督师范生在学习中的表现和进展；
Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) 为师范生提供必要的需求和用于学习活动的工具。
Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 教学方法Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

这个大纲强调了教学方法的运用，旨在使师范生成为学习的中心，使导师成为引导者。讲师将使用合作和综合的方法，帮助师范生掌握在小学汉语教学中的方法和技术运用。这些方法使师范生能够批判性思考、从各种来源获取知识并参与提供反馈。其他方法包括小组讨论、角色扮演、小组项目、思考-写作-分享-合作、综合练习、研究、故事创作、演示、叙述、各种游戏和其他相应的有助于适应学习环境的方法。此外，讲师应注意使用没有性别偏见的教学方法。建议讲师引导师范生在教学实践中创新并灵活运用教学方法，并师范生真实情况来选择教学工具。

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi na jumuishi kumwezesha mwalimu tarajali kumudu mbinu na matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina kwa shule za msingi. Mbinu hizo ni zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kufikiri kitunduizi, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho.

Mbinu hizo ni pamoja na majadiliano katika vikundi, igizo dhima, kazimradi, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, changanya kete, utafiti, utunzi wa hadithi, uwasilishaji, masimulizi, michezo mbalimbali na mbinu zingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji. Aidha, Mkufunzi anapaswa kuzingatia matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ambazo hazina dosari kwa mwitiko wa kijinsia. Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

## 8.0 教学工具/设备Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

讲师应该利用环境中可获得的工具，帮助师范生培养好奇心和探索精神、促进批判性思维、合作和沟通，并利用感官通道进行学习。教学工具应该帮助讲师理解所教授的内容。建议讲师利用周围环境中可获得的工具。其中一些工具包括实物、图片和图表、词典、触摸/操作工具、手语字母、点字机和信息技术辅助工具。教材的清单列表将由TET提供。

Mwalimu tarajali anapaswa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira au kufaragua zana ambazo zitamsaidia mwanafunzi kujenga tabia ya udadisi na ugunduzi; kukuza fikra tunduizi, ushirikiano, na mawasiliano, na kutumia milango ya fahamu katika ujifunzaji. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Baadhi ya zana hizo ni vitu halisi, picha na michoro, kamusi, zana mguso/mkwaruzo, alfabeti ya lugha za alama, mashine za breli na vifaa vya TEHAMA. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 学习进度评估Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

评估是教学过程中的重要问题。在汉语教学方法课程中，评估将与其他授课科目在教师培训学士阶段同时进行。这个评估能帮助教育师范学院评估师范生在相关课程中的能力水平。同时，它还能帮助师范生选择合适的教学和学习方法和工具来教学。发展性评估将根据每个学习活动中明确规定的标准进行。因此，评估工具包括练习、面对面问答、实验、访谈、课程文件、项目作业以及学期考试。此外，进行对师范生的发展性评估也是非常重要的，以便确定他们的能力发展程度。评估结果将有助于进行改进，以确保教育师范学院的教学目标得以实现。

培训师应设计更多评估活动来促进学习。期末考试将占70%，而持续评估将占30%。师范生至少需要在持续评估中获得50%的合格分数，并在期末评估中达到相同的标准才能获得证书。如果未能通过，师范生可以在三年内重复考试两次。表2显示了持续评估的分数分配。

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa lugha ya Kichina utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya stashahada ya ualimu. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali ili kujenga umahiri katika somo husika. Aidha, utamwezesha mwalimu tarajali kutumia mbinu na zana stahiki katika ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana zinazotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, kazi mradi pamoja na mitihani ya muhula. Vilevile, tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali ni muhimu kufanyika ili kubaini ni kwa kiasi gani anajenga umahiri uliokusudiwa. Matokeo ya tathimini yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya elimu ya ualimu yanafanikiwa.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji wa mwisho utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

表 2：**Jedwali 2:** 持续评估标志计划 *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | 评估活动 **Shughuli za upimaji** | 百分比分配 **Mgawanyo (%)** |
|---|---|---|
| 1 | 第一学年第一学期考试 Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | 第一学年期末考试 Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | 第二学年第一学期考试 Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | 项目任务 Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | 作品集 Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | 总分**Jumla** | **30** |

## 10.0 课时数量Idadi ya Vipindi

《小学汉语教学技能文凭培训大纲》根据特定技能的重要性和实习教师的任务活动，给出了教学所需的时间估计。这些时间估计是以课时为单位，每个课时为60分钟。该课程针对对师范生第一年和第二年的培训的课时数量为每周五节（5个）针对。

Muhtasari wa Somo la mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajari. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vitano (5) kwa wiki kwa mwaka wa I na II.

## 11.0 教学内容Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

教与学方法概要　汉语学科教学方法包含的内容排列在表3中。内容分为六个部分，即：主要能力、具体能力、教学活动、评估模式、教具和课时数量正如在表3和表4中所示。

Maudhui ya muhtasari yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele sita ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa na idadi ya vipindi.  Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 - 4

## 第一年Mwaka wa Kwanza

表 3： **Jedwali 3**：第一年教学内容 *Maudhui ya Ufundishaji na ujifunzaji kwa mwaka wa kwanza*

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 掌握小学汉语教学方法<br>Kumudu Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina katika Elimu ya Msingi | 1.1 分析小学汉语教学方法<br>Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina kwa Elimu ya Msingi | (a) 学习小学汉语教学方法<br>Kuaridhia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina katika elimu ya msingi | 描述小学汉语教学方法<br>Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zimearidhiwa | 摄像机、录音机、语言实验室、单词表、收音机、扬声器<br>Virekodi video, virekodi sauti, kadi za maneno, kipaza sauti, maabara ya lugha, orodha ya maneno, redio, spika | 29 |
| | 1.2 掌握基于年级层次的听力教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusikiliza kulingana na ngazi ya darasa husika | (a) 能够使用游戏来学习和教授听力技巧<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha stadi za kusikiliza | 展示对体育游戏在听力技能教学中的应用<br>Sanaa na michezo imetumiwa katika kufundisha stadi za kusikiliza | 摄像机、录音机、语言实验室、单词表、收音机、扬声器<br>Virekodi video, virekodi sauti, kadi za maneno, kipaza sauti, maabara ya lugha, orodha ya maneno, redio, spika | 23 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 在听力教学中能够运用不同的方法应对大班授课。<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za kusikiliza | 展示掌握使用各种方法向大班教授听力技巧<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |
| | | (c) 能够在听力技巧的学与教中使用时事热点方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za kusikiliza | 展示掌握将各种时事热点问题嵌入到听力技巧教学中的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 能够在听力技巧的教学中使用信息技术方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kusikiliza | 展示对将 (TEHAMA) 嵌入听力技能教学方法的掌握<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |
| | | (e) 能够使用其他学习和教授听力技巧的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za kufundisha stadi za kusikiliza | 展示掌握使用其他方法教授听力的能力<br>Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 掌握基于年级层次的口语教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kuzungumza kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika | (a) 掌握游戏在学习和教授口语技巧中的应用<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha stadi za kuzungumza | 游戏在口语技能教学中的应用与掌握<br>Sanaa na michezo imetumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza | 带有交叉引用的视频或音频<br>Vifaa vya michezo, video au sauti zenye masuala mtambuka | 23 |
| | | (b) 在口语教学中能够运用不同的方法应对大班授课<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za kuzungumza | 展示掌握使用各种方法向大班教授口语技巧<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) 掌握在口语技能教学中使用各种嵌入时事热点问题的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu mbalimbali za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za kuzungumza | 展示掌握将各种时事热点问题嵌入口语技能教学的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | | (d) 掌握信息通信技术TEHAMA在口语教学中的应用<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kuzungumza | 展示将信息通信技术TEHAMA 嵌入口语技能教学的方法的掌握<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |

| 主要能力 Umahiri mkuu | 具体能力 Umahiri mahususi | 教学活动 Shughuli za ujifunzaji | 评估模式 Vigezo vya upimaji | 教具 Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | 课时数量 Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) 掌握运用其他口语教学方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha stadi za kuzungumza | 展示掌握其他口语教学方法<br>Mbinu zingine za kufundisha stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | 1.4 掌握基于年级层次的语音教学方法<br>Kumudu Mbinu za kufundisha matamshi kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika | (a) 能够在语音的教学中使用游戏<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha wa matamshi | 展示对体育和游戏在语音教学中的应用掌握<br>Sanaa na michezo imetumiwa katika kufundisha matamshi | 带有交叉引用的视频或音频<br>Vifaa vya michezo, video au sauti zenye masuala mtambuka | 23 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 在语音教学中能够运用不同的方法应对大班教学<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha matamshi | 展示掌握使用各种方法向大班教授发音<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha matamshi zimetumiwa | | |
| | | (c) 能够结合时事热点进行语音教学<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha matamshi | 时事热点进行语音教学被结合<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha matamshi zimetumiwa | | |

| 主要能力 Umahiri mkuu | 具体能力 Umahiri mahususi | 教学活动 Shughuli za ujifunzaji | 评估模式 Vigezo vya upimaji | 教具 Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | 课时数量 Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 掌握信息通信嵌入技术TEHAMA在语音技巧教学中的运用 Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za matamshi | 展示掌握将 信息通信技术TEHAMA 嵌入语音教学的方法 Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | | (e) 掌握其他语音教学方法的运用 Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha matamshi | 展示对使用其他语音教学方法的掌握 Mbinu zingine za kufundisha stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.5 掌握基于年级层次的词汇教学方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha Msamiati kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika | (a) 掌握游戏在词汇教学中的运用<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha msamiati | 展示对体育和游戏在词汇教学中的应用掌握<br>Sanaa na michezo imetumiwa katika kufundisha msamiati | 带有交叉引用的视频或音频<br>Vifaa vya michezo, video au sauti zenye masuala mtambuka | 23 |
| | | (b) 能够在词汇教学中运用不同的方法应对大班教学<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha msamiati | 展示掌握使用各种方法向大班教授词汇<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha msamiati zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) 能够在词汇教学中运用时事热点嵌入各种问题的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mbalimbali mtambuka katika ufundishaji wa msamiati | 展示掌握在词汇教学中嵌入各种时事热点问题的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji wa msamiati zimetumiwa | | |
| | | (d) 掌握信息通信技术(TEHAMA)嵌入方法在词汇教学方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha msamiati | 展示掌握将 信息通信技术(TEHAMA) 嵌入词汇教学的方法<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha msamiati zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) 掌握其他词汇教学方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha msamiati | 展示对使用其他词汇教学方法的掌握<br>Mbinu zingine za kufundisha msamiati zimetumiwa | | |
| | 1.6 掌握基于年级层次的阅读教学方法<br>Kumudu Mbinu za kufundisha stadi za Kusoma kwa kuzingatia ngazi ya darasa husika | (a) 能够运用艺术和游戏来学习和教授阅读技巧<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha stadi za kusoma | 展示对体育和游戏在阅读技能教学中的应用的掌握<br>Sanaa na michezo imetumika katika kufundisha stadi za kusoma | 语言实验室、录音机，收音机、扬声器<br>Virekodi video, virekodi sauti, simu ya mkononi, kipaza sauti, maabara ya lugha, spika | 23 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 在阅读技巧教学中能够运用多种方式应对大班教学<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za kusoma | 展示掌握使用各种方法向大班教授阅读技巧<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za kusoma zimetumika | | |
| | | (c) 掌握在阅读技能教学中使用嵌入时事热点问题的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za kusoma | 展示掌握在阅读教学中嵌入各种时事热点问题的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za kusoma zimetumika | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 能够使用信息通信技术 TEHAMA 嵌入方法教授阅读技能<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kusoma | 展示掌握将信息通信技术 TEHAMA 嵌入阅读技能教学的方法<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za kusoma zimetumiwa | | |
| | | (e) 掌握使用其他方法教授阅读技巧<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha stadi za kusoma | 展示对使用其他方法教授阅读技巧的掌握<br>Mbinu zingine za kufundisha stadi za kusoma zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.7 掌握基于年级层次的写作教学方法<br>Kumudu mbinu za kufundisha stadi za uandishi kulingana na ngazi ya darasa husika | (a) 能够使用艺术和游戏来学习和教授写作技巧<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha stadi za kuandika | 展示对体育和游戏在写作技巧教学中的应用的掌握<br>Sanaa na michezo imetumika katika kufundisha stadi za kuandika | 运动器材、参考书、带交叉引用的录像机或录音机<br>Vifaa ya michezo, video au vinasa sauti vyenye masuala mtambuka | 23 |
| | | (b) 在写作技巧教学中能够运用不同的方法应对大班教学<br>Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za uandishi | 展示掌握使用各种方法向大班教授写作技巧<br>Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika kufundisha stadi za uandishi zimetumiwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) 能够使用将各种时事热点问题嵌入教学写作技巧的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mbalimbali mtambuka katika kufundisha stadi za uandishi | 展示掌握将各种时事热点问题嵌入到写作技巧教学中的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha stadi za uandishi zimetumiwa | | |
| | | (d) 能够在写作技巧教学中使用信息通信技术TEHAMA嵌入方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za uandishi | 展示将 信息通信技术TEHAMA 嵌入写作技能教学的方法<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha stadi za uandishi zimetumika | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**Zana /Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) 掌握运用其他方法教授写作技巧<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha stadi za uandishi | 展示对使用其他方法教授写作技巧的掌握<br>Mbinu zingine za kufundisha stadi za uandishi zimetumika | | |
| | 1.8 能够在教学中使用技术和其他工具<br>Kumudu matumizi ya teknolojia na vyombo vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) 掌握在线平台在改进教学方面的应用<br>Kumudu matumizi ya majukwaa ya kimtandao katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji | 正确使用在线平台以改善教学<br>Matumizi sahihi ya majukwaa ya kimtandao katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji yametumiwa | 投影仪、麦克风、语言实验室、记号笔、收音机、扬声器<br>Virekodi video, virekodi sauti, simu za mkononi, kipaza sauti, maabara ya lugha, spika | 23 |
| | | (b) 提高在教学中使用技术和其他辅助工具的能力<br>Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | 展示掌握在教学中使用技术和其他辅助媒体的技能<br>Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji vimetumiwa | | |

## 第二年Mwaka wa Pili

表 4：**Jedwali 4:** 第二年教学内容 *Maudhui ya Ufundishaji na ujifunzaji kwa mwaka wa pili*

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**vifaa/Zana** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 掌握小学汉语教学方法<br>Kumudu Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kichina katika Elimu ya Msingi | 1.1 掌握基于年级层次的语法教学方法<br>Kumudu Mbinu za kufundisha Sarufi kwa kuzingatia ngazi za darasa husika | (a) 掌握游戏在语法教学中的运用<br>Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika kufundisha sarufi | 展示对体育和游戏在语法教学中的应用的掌握<br>Sanaa na michezo imetumika katika kufundisha sarufi | 带有图表的文章解释语法教学技巧，使用投影仪或黑板展示技巧<br>Nakala zenye michoro inayoelezea mbinu za kufundisha sarufi | 23 |
| | | (b) 能够在大班中使用不同的方法教授语法<br>Kumudu matumizi ya mbinu mbalimbali za kufundisha sarufi katika darasa kubwa | 展示掌握使用各种方法向大班教授语法<br>Mbinu mbalimbali za kufundisha sarufi katika darasa kubwa zimetumika | | |
| | | (c) 能够在语法教学中使用嵌入各种时事热点问题的方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mbalimbali mtambuka katika kufundisha sarufi | 展示掌握在语法教学中嵌入各种时事热点问题的方法<br>Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika kufundisha sarufi zimetumika | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 教学活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 评估模式<br>**Vigezo vya upimaji** | 教具<br>**vifaa/Zana** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 能够在语法教学中使用TEHAMA嵌入方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha sarufi | 展示对将 TEHAMA 嵌入语法教学的方法的掌握<br>Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika kufundisha sarufi zimetumika | | |
| | | (e) 能够使用其他语法教学方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu zingine za kufundisha sarufi | 展示对使用其他语法教学方法的掌握<br>Mbinu zingine za kufundisha sarufi zimetumika | | |
| | 1.2 掌握协调课外活动的各种方法<br>Kumudu matumizi ya mbinu mbalimbali katika kuratibu shughuli za nje ya darasa | (a) 能够运用多种方式协调课外活动<br>Kumudu matumizi ya mbinu mbalimbali katika kuratibu shughuli za nje ya darasa | 展示对协调课外活动的各种方法的应用掌握<br>Mbinu mbalimbali za kuratibu shughuli za nje ya darasa zimetumika | 显示课外活动的图片或包含课外活动的视频<br>Michoro yenye kuonesha mbinu za kuratibu shughuli nje ya darasa au video zenye shughuli za nje ya darasa | 23 |

## 参考文献Bibliografia


Cai, Y. Q. (2013). *Intermediate Chinese writing course*. Beijing Language and Cultural University.

Chu, G. M., et al. (2016). *Intermediate comprehensive course*. Beijing Language and Cultural University.

Chu, G. M. (2011). *Elementary comprehensive course*. Beijing Language and Cultural University.

Cambridge Local Examination Syndicate, corporate (2022). *Cambridge IGCSE Chinese as a Second Language 0523 syllabus for 2023, 2024 and 2025*. Retrieved from www.cambridgeinternational.org/igcse

NSW Education Standards Authority (NESA), corporate (2017). *Chinese K–10 Syllabus*. Retrieved from www.educationstandards.nsw.edu.au

Jiang, L., et al. (2013). *Standard Course HSK LEVEL 1*. Beijing Language and Cultural University Press.

Li, X. Q. (2003). *Kuaile Hanyu. Secondary school Book One*. Beijing Language and Cultural University.

Li, L. X. (2024). *Dictionary of 5000 graded words for new HSK (Level 4&5)*. Beijing Language and Cultural University.

Li, L. X. (2024). *Dictionary of 5000 graded words for new HSK (Level 1,2&3)*. Beijing Language and Cultural University.

Moodley, P. (2015). Student overload at university: large class teaching challenges: part 1. *South African Journal of Higher Education*, 29(3), 150-160.

Mugabe, L., & Ndayambaje, I. (2022). The implications of large classes on active learning at University of Rwanda-College of Education. *Rwandan Journal of Education, 5*(2).

Olajide, J. O. (2012). Teaching Science for Better Achievement in Large Classes. *International Journal of African Studies*.

Zhang, J. (2002). The survey and analysis of big class English teaching. *Journal of North China Institute of Water Conservancy and Hydroelectric Power (Social Sciences Edition)*, 18(4), 92-94.

Zhang, L. (2010). Problems of teaching English in primary large classes in rural areas and application of group study. *Journal of Guangxi Normal University for Nationalities*, 27(1), 129-131.